

## Kuvuna

*Mollucella* huchukua muda wa siku 80 hadi 90 kuanzia kupanda hadi kuvuna. Wakati wa kuvuna matawi huwa na urefu wa sentimita 50 hadi 80.

- Ni vyema kukata ukitumia kisu chenye makali, asubuhi au jioni ili kuimarisha uhai wa ua.
- Tia matawi yaliyokatwa ndani ya ndoo yenye maji.
- Mavuno yanayotarajiwa ni matawi mawili matatu kwa kila mmea.

## Kuchagua

Kutenga na kuosha ni lazima kufanywe kabla ya kuchagua.

- Matawi yanasafishwa kwa kutoa majani yaliyo kati ya *caylxes* ili kufanya maua yaonekane vizuri.
- Matawi mafupi na yaliyoharibika hutupwa na yale mazuri yanatiwa kwenye *disulphide solution*(STS) ili kuimarisha uhai wa ua.

## Kupakia

- Matawi hutwiwa kwenye vijisanduku kulingana na ukubwa, nambari ya vitita na mpangilio wa kufunga.
- Ni lazima vichwa vya maua viwe sentimita 10 mbali na kijisanduku ili kuzuia kuvunjika au kuharibika.



### Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P. 57811, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344

Baruapepe: resource.centre@kari.org

Tovuti: www.kari.org

#### Mtayarishaji:

Gateri, M.W.

#### Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

#### Mkuu wa Kituo,

KARI - Thika

S.L.P. 220, THIKA

Simu: (067)21281/521134 au: 2055038

Nukulishi: (067) 21285

Baruapepe: karithika@africaonline.co.ke

Vijitabu vya KARI vya taarifa, nambari / 5 /2008

**Shilingi 20 za Kenya**

# Ukuzaji wa ua la *molucella* la kukatwa



## Utangulizi

*Moleculla* au 'Kengele za Ireland' ni mmea wa mwaka ambao unatambuliwa sana kwa *calyxes* za rangi ya kijani kibichi, na zenye umbo la pia. *Moleculla* ni ua maarufu na linalopendekezwa sana katika soko la kimataifa la kuuzia maua.

## Mahitaji ya kimazingira

- *Moleculla* hukua vizuri zaidi katika ardhi zilizo katika urefu wa mita kati ya 1,500 hadi 1,800 juu ya usawa wa bahari na kipomo cha joto nyusi 15 hadi 20.
- *Moleculla* huhitaji mvua ya kutosha lakini hata ikinyunziwa bado hukua vizuri.
- Ukuzaji hupendekezwa zaidi kwa mchanga uliochimbwa kwa undani, ambao unapenyeza maji vizuri na wenye rutuba ya hali ya juu.



**Calyx zenye umbo la pia**

## Mbinu za ukuzaji

### Uzalishi

Mbegu hupandwa mashambani mara moja au kukuzwa pembeni kwanza.

- Kiwango cho joto mwafaka ni nyuzi 20 kwa muda wa wiki 3.
- Ili kuimarisha kuota, mbegu zinawewekwa kwenye baridi nyuzi 10, kwa siku 3.
- Kuhamisha mimea kupeleka shambani kunafanywa mimea chipukizi ikiwa na urefu wa sentimita 4 hadi 5. Mbegu zinazopandwa mashambani moja kwa moja zisifunikwe sana kwa sababu mwangaza ni muhimu katika kuota.



**Young molucella plant**

## Utayarishaji shamba

Shamba linachimbwa kwa undani hadi mchanga uachane.

- Tayarisha vitanda vya kupandia vya sentimita 100 vikiwa na vinjia vya sentimita 50 katikati. Vitanda vinafaa kuinuliwa kati ya sentimita 10 hadi 15 ili mchanga upitishwe maji ifaavyo.
- Ongeza mbolea iliyokomaa vizuri mchangani kiasi cha tani 20 kwa eka.

## Upandaji

- Upandaji wa mbegu au miche huhitaji nafasi ya sentimita 15 kati ya mimea na sentimita 25 kati ya mishororo.
- Tia mbolea ya DAP/TSP kiasi cha gramu 50 kila mita jumla.
- Uzididisha kiasi cha Nitrogen kwani hii huzambabisha mti kupata nguvu zaidi zaidi na kupunguza maua.

## Kuzuia magugu

- Kupalilia ili kuondoa kwekwe kunahitajika kila mara na kusiwe kwa kuchimbua undani.

## Unyunyizaji

- Kunyunyizia kwa njia ya (matone) *drip* ni njia mwafaka ya kulowesha mchanga. Hakikisha kuwa maji unayotumia ni safi.

## Kuchuna

- Chuna ncha ya mmea ili kuhimiza matawi kutokeza na kuimarisha afya ya mmea unpohitimu wiki 4 hadi 6.

## Uzuiaji wa maradhi

- *Botrytis* ni maradhi sugu yanayodhihirishwa na kufa kwa pembe za majani na matawi kugeuka kuwa rangi manjano. Yanaweza kuzuiwa kwa kutumia dawa za wadudu kama vile Bayleton.

## Kuwakinga wadudu

- *Cutworms*, *thrips* na *aphids* ni wadudu wanaoathiri *moleculla* zaidi. Dawa kama Brigade, Karate na Confidor huzuia wadudu hawa.